**MASOMO YA BIBLIA KWA NJIA YA POSTA**

**Karatasi ya Maswali: namba 12.**

Jaribu kuyajibu maswali yafuatayo kwa maneno yako mwenyewe. Pale palipoandikwa ‘Kazi ya ziada’, unaweza kulijibu swali kama unapenda, au kuliacha kama unaona ni gumu mno. Tafadhali jaribu kuyajibu maswali mengine yote.

**MASOMO: 45-48**

37. (a) Amri iliyo kubwa kabisa ni ipi?
 (b) Tunaweza kutamani kuwa matajiri na wenye nguvu?
 (c) Utumwa unakubalika kwa Mungu?
 (d) Tunapaswa kufanyaje kama wakubwa wetu wa kidunia wanatutaka tufanye kitu?

Kazi ya ziada
 (e) Kama ndugu yetu anafanya jambo lisilofaa, tufanyeje?

38. (a) Yesu alimtumia Msamaria katika mfano wake wa Msamaria-mwema. Kwa nini?
 (b) Toa mifano ya mahali Yesu alipoonesha huruma.
 (c) Yesu alikuwa na maana gani alipomwambia Petro, ‘chunga kondoo zangu’?
 (d) Upendo ni nini?

Kazi ya ziada
 (e) Mungu anasemaje juu ya vita vya wenyewe kwa wenyewe na mauaji ya kimbari?

39. (a) Mateso ni nini?
 (b) Mateso yaliletwa katika Bustani ya Edeni, kwa nini?
 (c) Mungu anasababisha mateso?
 (d) Kwa nini Mungu ‘anaturudi’?

Kazi ya ziada
 (e) Mateso yanatokea tu kwa bahati mbaya?

40. (a) Hebu toa mifano ya Kibiblia kuonesha mahali watu walipoishi kwa hofu.
 (b) Hebu elezea historia ya Wayahudi baada ya kutawanywa, mwaka 70 Baada ya Kristo.
 (c) Wakristo waliwahi kuteswa?
 (d) Yesu aliwahi kuahidi kuwa maisha yetu yasingekuwa na shida?

Kazi ya ziada
 (e) Hebu eleza matatizo uliyonayo katika maisha yako, na useme ni kwa nini unafikiri unayapata.

*Kumbuka kuweka jina lako, anwani na namba yako ya kumbukumbu katika karatasi yako ya majibu.*